END TB

# AZIMIO LA KISIASA KATIKA MKUTANO WA BALAZA KUU LA UMOJA WA MATAIFA JUU YA KIFUA KIKUU ULIOFANYIKA NEWYORK MAREKANI MWAKA 2018



eannaso
NTLP NATIONAL TUBERCULOSIS & LEPROSY PROGRAMME
Tanzania TB Community Network
Stop TB Partnership hosted by UNOPS

## UTANGULIZI

Sehemu hii inatoa taarifa na takwimu zinazohusiana na Mkutano wa Balaza kuu la Umoja wa Mataifa juu ya TB juu ya malengo na ahadi muhimu za Kifua kikuu kwa 2022 kama ilivyoanishishwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Kifua Kikuu

## MSIMAMO NA AHADI ZA AZIMIO LA KISIASA KATIKA MKUTANO WA BALAZA KUU LA UMOJA WA MATAIFA JUU YA KIFUA KIKUU

Ili kutokmeza Kifua Kikuu kabisa ni lazima kutokomeza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu, kuzuia maambukizi, na madhara mengine yatokanayo na Kifua Kikuu. Tunaweza kufikia malengo ya kutokomeza Kifua Kikuu, lakini tunahitaji nguvu ya pamoja kitaifa na utashi wa kisiasa kufikia malengo hayo. Utashi wa kisiasa unajidhihirisha kupitia Mkutano wa Balaza kuu la Umoja wa Mataifa wa Kifua kikuu ulifanyika tarehe 26 Septemba 2018 mjini New York Marekani. Mkutano huu uliudhuriwa na viongozi wa mataifa mbalimbali. Katika mkutano huu, Kifua Kikuu kilitajwa kuwa ni janga kubwa sana la kidunia na viongozi wa serikali walikubaliana kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kutokomeza janga hili. Moja ya agenda katika mkutano huo ilikua ni kukubali kwa viongozi wa serikali juu ya upatikanaji nafuu katika kuzuia, kutambua wagonjwa na matibabu ya Kifua Kikuu katika nchi zao. Agenda ya pili ilikua ni kuongeza kasi ya kutosha na endelevu ya kitaifa na kimataifa ya ukusanyaji fedha na utekelezaji wa utoaji wa huduma katika kupambana na Kifua Kikuu.

### KWA PAMOJA VIONGOZI WA SERIKALI WALIOHUDHURIA MKUTANO HUO IKIWEMO TANZANIA WALIAHIDI KUFANYA MAMBO KUMI KAMA IFUATAVYO;

#### TUNAHIDI KUTOA HUDUMA ZA UCHUNGUZI NA MATIBABU

1. kwa lengo la kutibu watu milioni 40 wenye Kifua Kikuu kufikia 2022.
2. kwa lengo la kutibu watoto milioni 3.5 wenye Kifua Kikuu kufikia 2022.
3. kwa lengo la kutibu watu milioni 1.5 wenye Kifua Kikuu sugu, ikiwa ni pamoja na watoto 115,000 wenye Kifua Kikuu sugu kufikia 2022.

#### TUNAAHIDI KUZUIA MAAMBUKIZI YA KIFUA KIKUU

4. Kwa wale walio katika hatari zaidi ya kuugua ili angalau watu milioni 30, ikiwa ni pamoja na watoto chini ya miaka mitano milioni 4, kaya milioni 20 za watu walioathirika na Kifua Kikuu, na watu milioni 6 wanaoishi na VVU, wanapata matibabu ya kuzuia Kifua Kikuu kufikia 2022.

#### TUNAHIDI KUTENGA FEDHA ZA KUTOSHA

5. kwa ajili upatikanaji huduma bora za kuzuia, kufanya uchunguzi na matibabu ya Kifua Kikuu kwa lengo la kuongeza uwekezaji wa angalau dola bilioni 13 kwa mwaka katika kutokomeza Kifua Kikuu kufikia 2022.
6. kwa nia ya kuongeza uwekezaji wa jumla ya dola bilioni 2 za Marekani, ili kufikia pengo la wastani wa dola milioni 1.3 za fedha kwa kila mwaka kwa ajili ya uchunguzi wa Kifua Kikuu, kuhakikisha kwamba nchi zote zinachangia kwa ufanisi katika utafiti na maendeleo.

#### TUNAAHIDI KUHAMASISHA NA KUUNGA MKONO JITIHADA ZA KUTOKOMEZA UNYANYAPAA NA UBAGUZI WA AINA YOYOTE KWA WATU WENYE KIFUA KIKUU

7. ikiwa ni pamoja na kuondoa sheria, sera na mipango inayowabagua watu wenye kifua kikuu, kulinda na kukuza haki za binadamu na heshima. Kutambua vikwazo mbalimbali vya kijamii na utamaduni vinavyochangia kushindwa kuzuia ugonjwa wa kifua kikuu, uchunguzi na huduma za matibabu, hususani kwa wale walio katika mazingira magumu au katika hali magumu, na haja ya kuunda huduma za afya shirikishi zinazozingatia mgonjwa, jamii na jinsia na haki za binadamu.

#### TUNAAHIDI KUTOA HUDUMA KWA HARAKA IWEZEKANAVYO, HUDUMA MPYA ZILIZO SALAMA, KWA UFANISI, USAWA, GHARAMA NAFUU, NA UPATIKANAJI WA MADAWA.

8. sehemu ya huduma na uchunguzi rafiki kwa watoto, madawa salama na madhubuti na madawa ya muda mfupi ya kutibu watu wazima, vijana na watoto kwa aina zote za kifua kikuu na maambukizi, pamoja na ubunifu ili kuimarisha mifumo ya afya kama vile zana za mawasiliano na mifumo ya teknolojia mpya na zilizopo, ili kuwezesha mfumo jumuishi wa kuzuia maambukizi, matibabu na huduma za kifua kikuu.

#### TUNAAHIDI KUMUOMBA MKURUNGEZI MKUU WA SHRIKA LA AFYA DUNIANI KUENDELEA KUTENGENEZA MFUMO WA UWAJIBIKAJI KISECTA.

9. na kuhakikisha utekelezaji wake kwa wakati kufikia mwaka 2019.

#### TUNAHIDI KUMUOMBA KATIBU MKUU KWA KUSHIRIKIANA NA SHIRIKA LA AFYA DUNIANI KUTOA TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2020

10. juu ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa katika sekta zote, ili kuongeza kasi ya kufikia malengo ya Kifua Kikuu yaliyowekwa, ambayo yatatoa taarifa ya maandalizi ya mapitio ya kina na wakuu wa nchi na serikali katika mkutano wa ngazi ya juu wa mwaka 2023.

## MALENGO YA AZIMIO LA KISIASA JUU YA KIFUA KIKUU

Azimio la kisiasa katika Mkutano wa Balaza kuu la Umoja wa Mataifa juu ya Kifua Kikuu liliweka malengo kadhaa ya kidunia yaliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi, ikiwa ni pamoja na malengo ya kutibu watu milioni 40 wenye Kifua Kikuu kuanzia mwaka 2018 hadi 2022, watoto wenye Kifua Kikuu milioni 3.5, watu milioni 1.5 wenye Kifua Kikuu sugu na kuhakikisha angalau watu milioni 30 wanawekwa matibabu ya Kinga ya Kifua Kikuu.

Ili kufanya utekelezaji wa malengo haya ya kidunia uwe rahisi katika ngazi ya kitaifa kwa lengo la kuendeleza utashi wa kisiasa kitaifa, kuwezesha ufuatiliaji na uwajibikaji, Shirika la Stop TB Partnership limetoa mgawanyo malengo haya kwa kila nchi kwa kutumia taarifa zinazokusanywa na WHO kutoka nchi wanachama. Makadirio haya yamefanywa kwa kutumia mfumo wa TIME uliotekelezwa na Avenir Health. Kwa nchi ambazo zina wagonjwa wengi, Mpango mkakati wa taifa wa kifua Kikuu na malengo ya mfumo wa utendaji wa Global Fund vilitumika. Malengo ya Tanzania ni kama ifuatavyo;

### MALENGO YA UTAMBUZI NA MATIBABU YA KIFUA KIKUU KWA WATOTO

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 10,700 | 14,500 | 18,600 | 17,700 | 16,600 | 78,100 |

### MALENGO YA UTAMBUZI NA MATIBABU YA KIFUA KIKUU SUGU

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 409 | 576 | 1,200 | 1,700 | 1,800 | 5,685 |

### MALENGO YA KINGA KUZUIA KIFUA KIKUU (PREVENTATIVE THERAPY) KWA WALIOKARIBU (CONTACTS) NA WATOTO CHINI YA MIAKA MITANO

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 5,440 | 14,370 | 26,770 | 33,660 | 39,750 | 119,990 |

### MALENGO YA KINGA KUZUIA KIFUA KIKUU (PREVENTATIVE THERAPY) KWA WALIOKARIBU (CONTACTS) NA WATOTO ZAIDI YA MIAKA 5

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 5,896 | 12,171 | 33,149 | 56,015 | 69,540 | 176,771 |

### MALENGO YA KINGA KUZUIA KIFUA KIKUU (PREVENTATIVE THERAPY) WATU WANAOISHI NA VVU

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 291,813 | 77,925 | 88,237 | 64,004 | 51,964 | 573,943 |

### MALENGO YA UTAMBUZI NA MATIBABU YA KIFUA KIKUU

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 75,800 | 101,000 | 124,000 | 115,200 | 107,000 | 523,000 |

MALENGO YA KINGA YA KUZUIA KIFUA KIKUU

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 303,150 | 104,460 | 148,160 | 153,680 | 161,250 | 870,700 |

RASILIMALI ZINAZOHITAJIKA ILI KUFIKIA MALENGO YA MKUTANO WA BALAZA KUU LA UMOJA WA MATAIFA JUU YA KIFUA KIKUU (US$)[1,2,3]

| MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiasi ($) | 84,484,413 | 103,493,380 | 148,120,779 | 163,280,006 | 166,065,806 | 665,444,385 |

## NINI KINACHOTAKIWA KUFANYIKA KUONGEZA ILI KUFIKIA MALENGO YA MKUTANO WA BALAZA KUU LA UMOJA WA MATAIFA JUU YA KIFUA KIKUU?

- Kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya shughuli za Kifua Kikuu nchini. Serikali itenge rasilimaji za kutosha kwa ajili ya afua za kutokomeza Kifua Kikuu (Uibuaji wa wagonjwa, dawa and vitendanishi);
- Kuimarisha utashi wa kisiasa na kuongoza mapambano dhidi ya Kifua Kikuu katika ngazi zote za uongozi. Na Kifua Kikuu iwe ajenda ya kudumu katika mikutano ya kisiasa na ya kijamii;
- Tatizo la Kifua Kikuu ni mtambuka kushughulikia kunahitaji ushiriki wa sekta zote. Sekta zote za umma zihusike katika mapambano dhidi ya janga la Kifua Kikuu (Kazi na ajira, Nishati na Madini, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Uhamiaji, Elimu na Magereza). Sekta binafsi, Asasi za kiraia, Mashirika yasiyo ya kiserikali na makundi mengine ya kijamii yajumuishe vita dhidi ya Kikuu katika mipango yao na kuongoza harakati za mapambano hayo;
- Kuongeza upatikanaji wa huduma za upimaji angalau katika vituo vyote vya afya nchini;
- Kuimarisha kampeni za uhamasishaji na uraghibishi ili kuongeza uelewa kwa jamii hasa kwenye maeneo ya makazi duni kwenye miji mikubwa, migodini na jamii za wavuvi;
- Bunge liimarishe mtandao wa wabunge Tanzania (Parliamentary TB Caucus) na kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kama ilivyoazimiwa na baraza la mabunge duniani; na
- Viongozi katika ngazi zote za serikali waongoze kikamilifu katika vita dhidi ya Kifua Kikuu.

## MAREJEO


WHO Global TB Report 2019
Stop TB Partnership - *http://www.stoptb.org/resources/cd/*
Shirika la Afya Duniani *(www.who.int/tb)*
Stop TB Partnership *(www.stoptb.org)*
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma *(www.ntlp.co.tz)*

## NOTES

## WASILIANA NA NASI

Tanzania TB Community Network (TTCN)

Hosted by EANNASO

Plot # 1 Olorien, Kijenge | Off Njiro Road

P.O Box 6187 | Arusha, Tanzania

+255 739 210598 ttcn.tanzania@gmail.com ttcntanzania